COUNTY ASSEMBLY OF MOMBASA
THE HANSARD

Tuesday, 14th February, 2023
Third Assembly – Sixth Sitting

[The County Assembly met at 2:45p.m. at the County Assembly Buildings]
[The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Mwalimu Makarani) in the Chair]

PRAYERS

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani)**:** Have your seats Honourable Members. Yes Clerk?

MOTION

PARTNERSHIP BETWEEN COUNTY GOVERNMENT TO BUILD THE CAPACITY OF YOUTH, TUK TUK AND BODA BODA DRIVERS

Yes, Honourable Amriya Boy?

Hon. Amriya Juma: Thank Mr. Speaker. I beg to move the following Motion on partnership between County government to build the capacity of youth, tuk tuk and boda boda drivers.

AWARE that, Article 55 of the Constitution of Kenya, 2010 mandates the State, (The National and County governments) to take measures including affirmative action programs to ensure the youth get basic education and training;

FURTHER AWARE there had been rampant flouting of traffic laws which have ended in accidents occasionally leading to fatalities and injuries;

NOTING THAT there is tremendous skills gap found in youth, Tuk Tuk and Boda boda drivers that needs to be bridged for their benefits and the society at large;

CONCERNED that failure to impart the necessary skills to this sector of the society may occasion heavy human toll and unintended negative consequences to the public;

I, therefore urge this Assembly to resolve:

THAT the County government to partner with private sector players and stakeholders to organize financial management, entrepreneurial, legal and other skills to build the capacity of the youth, Tuk tuk and Boda boda drivers.

I humbly request Honourable Juma to second.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani)**:** Yes, Honourable Juma?

Hon. Juma Mwalimu: Thank you Mr. Speaker Sir. I stand to second the Motion.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani)**:** Honourable Members, I propose a question on the Motion on partnership between the County government to build the capacity of youth, Tuk tuk and Boda boda drivers be debated in this House.

[Question proposed and agreed to]

Yes, Honourable Amriya?

Hon. Amriya Juma: Ahsante sana Bwana Mwenyekiti. Hoja hii imefika mbele ya Jumba hili kwa sababu tumeangalia kwamba takwimu ya vijana wetu wingi wako kwa biashara ya hizi boda boda na tuktuk asilimia 60 wako katika biashara hii na pia Mombasa watumiaji wa mfumo huu wa usafiri wa bodaboda na tuktuk ni asilimia kubwa sana Bwana Mwenyekiti. Kwa hivyo ukiangalia pia zile kesi za ajali ambazo nyingi zinasababishwa na mfumo huu wa usafiri Mheshimiwa, ukiangalia hata katika hospitali kuu yetu ya Coast General utaona kwamba kuna wadi imewekwa yaani tofauti ili watu wa bodaboda waweze kuhudumiwa. Bwana Spika, inajulikana wadi namba saba ni ya bodaboda, kwa hivyo ni muhimu sana hawa ndugu zetu maana yake wanatumia usafiri huu kusafirisha watoto wetu kuenda shule na wazazi wetu na jamii kwa jumla tuweze kuweka mfumo ambao wataweza kuwa na sheria maalum ambapo mwanzo tutawafundisha mafunzo zaidi kuhusu usafiri, yaani kimombo *traffic rules* ambazo wanaweza kufuatilia pia tutafute wafadhili ambao pia wanaweza pia kuangalia kwamba wanafuatilia zile sheria ya kuangalia vile vidhibiti, kuangalia pia nidhamu yao. Hivyo basi, mimi nimeleta hoja hii kwamba hatuna sheria yoyote kuhusu mambo na hawa ndugu zetu wa tuktuk na bodaboda ila tu kuwatoza hayo mambo ya leseni. Kwa hivyo ningependa serikali Gatuzi iangalie hii sekta ya usafiri tutafute wafadhili na kunao ambao wamejitokeza lakini vile hatuna sheria yoyote ndio nimeamua kuleta Mswada huu ili wawe na nguvu kuja kusaidia huu mfumo wetu wa usafiri. Kwa hivyo naomba Bunge hili liweze kupitisha Mswada huu ili uweze kusaidia jamii yetu. Shukran sana Bwana Spika.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Mwalimu)**:** Thank you Honourable Amriya. Yes, Honourable Leila Nyache?

Hon. Nyache: Ahsante sana Mheshimiwa Spika na mimi kuweza kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu, pili nampongeza Mheshimiwa mwenza Amriya juma Boy aliyekuja na hoja hii; kusema la kweli Mheshimiwa Spika vijana wetu hawa wanaoendesha hizi bodaboda wengi wao huwa hawana vibali na huwa sana wanasababisha ajali na ni ajali nyingi sana ambazo tumezishuhudia na tunaomba vile alivyosema kwamba tutafute wafadhili waweze kushirikiana na serikali yetu ya Kaunti.

Tutafute pia wadhamini waweze kushirikiana tuweze kuwapatia watoto wetu elimu ya kuwa barabarani na kuendesha hizo bodaboda zao na waweze kujua sheria za barabarani ndio hapo wataweza kupunguza hizo ajali. Nimesimama kuunga mkono. Ahsante Mheshimiwa Spika.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani)**:** Yes, Honourable Juma Mwalimu?

Hon. Juma Mwalimu: Ahsante Bwana Spika kwa kunipatia fursa hii. Mimi nimesimama kumuunga mkono Mheshimiwa mwenza Bi. Amriya Juma Boy na kulingana na bodaboda wapelekaji tuktuk hawana ujuzi wa kupeleka tuktuk hizo; utaona mtu amejifunza tu siku moja tayari siku ya pili kesho ameingia barabarani na hususan kuiangalia hawa wapelekaji tuktuk mtu akiona abiria tu upande ule wa pili utamuona anapiga *u turn* bila kuwasha hata zile zinazoitwa…

[Laughter]

…*indicators* tayari utamshtukizia tu apiga *u turn* na huku nyuma kumbe kunakuja pikipiki ama gari utashtukizia tu ajali imepatikana. Kwa hio hawa watu wakipata mafunzo bora itakuwa ni bora zaidi kwa sababu pia itapunguza zile ajali za barabarani. Naunga mkono Mswada huu na ahsante sana Bwana Spika kwa kunipa fursa hii.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani)**:** Thank you. Honourable Manuari?

Hon. Juma Manuari: Ahsante Bwana Spika na nichukue nafasi hii kwanza kushukuru Mwenyezi Mungu; pili kumuunga mkono dadangu wakili mwenza, dadangu Amriya Boy. Mheshimiwa Spika kutokana na hoja hii ya dadangu aliyoileta mimi nimuunge mkono na nimuongezee kumuambia katika wale watu tunao watafuta kuhakikisha wanasaidiana na serikali ya Kaunti kuhakikisha tunasomesha vijana wetu katika maswala ya sheria barabarani mimi ningependekeza ya kwamba wale wauzaji wa hizi pikipiki ambazo zinaitwa bodaboda ama muuzaji wa tuktuk kabla mtu hajanunua ile tuktuk kama ni tajiri amekuja nunua kupeleka biashara kwa watu wake basi ni muhimu kwa yule muuzaji wa vitu kama vile atengewe sheria katika hii Bunge letu aambiwe ya kwamba kabla hajamuuzia pikipiki mtu amchukue ampe mafunzo kwa sababu tukisema hili Jumba letu ama hii Kaunti na huu mfuko wetu tulio nao tuwe tutagharamia ama tutasimamia majukumu ya kuwasomesha hawa vijana wa bodaboda kusema ukweli tutakuwa hapo ni kurundika lawama katika Kaunti yetu.

Kwa hivyo mimi kwa kumuongezea dadangu nimuunge mkono na nimuambie kuwa katika maswala ambayo yapo tuwape nafasi wale wauzaji tuwawekee kama ni sheria kupitia Kaunti kabla hujamuuzia mtu pikipiki aletwe yule kijana amlipie kile kima atakacholipa afanyiwe mtihani asomeshwe sheria za barabara ili akitoka pale tutakuwa tunapunguza ile namba ya wale walikuwa tayari washanunua ndio nasi tupate nafasi kuwatafuta walewaliobakia kando ili tuwaenue. Kwa hayo mengi na machache ahsante Mheshimiwa Spika.

[Applause]

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani)**:** Yes, Honourable Katana?

Hon. Katana: Mheshimiwa Spika ahsante kwa kunipa nafasi hii. Mtanisamehe naweka karatasi juu na nikirudisha chini kwa sababu nina mafua Mheshimiwa Spika, sasa uoga wangu naona kama ambaye nikifanya hivi kuna vitu naweza dondosha.

Mheshimiwa Spika nataka kuchangia katika swala hili la kuwahusu madereva wa tuktuk na maboda boda; ni kwamba hata katika *Finance Bill* ile tulipitisha tumeona tumewawekea kwamba watakuwa wakilipa shilingi 200 na uoga wangu ni kwamba tunawatoza watu ambao hata hawana vibali vya kuendesha hivi vitu sasa kama serikali ya Kaunti ya Mombasa. Mheshimiwa Spika ni kama ambaye sisi tumekuwa tukichangia pakubwa na kutafuta ushuru kwa watu ambao hawana idhini na vibali kufanya biashara hii. Kwa hivyo katika kupiga upondo hili swala ambalo Mheshimiwa wa Mjambere amelileta ni kwamba itakuwa vyema kama serikali ya Kaunti hii ya Mombasa italifanya hili kwa haraka iwezekanavyo ili mbali na kuwapa mafunzo itakuwa pia tumewasaidia kiasi cha kwamba hata zile kampuni zinazotoa bima zitakuwa zina faida kwao, kwa sababu kama hauna vibali na hata pikipiki ikiwa na bima maana wewe huna kibali cha kuendesha basi bima ile itakuwa ya bure maana haitakulipa Mheshimiwa Spika. Swala lengine ni kwamba katika hili swala la ndugu la hawa zetu wa bodaboda na tuktuk watakapo fanyiwa hivyo ya kupewa mafunzo haya mimi nasema itakuwa ni vizuri pia waweze kuwezeshwa hata kama tutakuwa na mwamvuli mmoja ambao najua tayari iko Sacco ya bodaboda wote na watu wa tuktuk ili zaidi ya kuwapa mafunzo pia wakaweze kuwa katika Sacco zao ili serikali ya Kaunti hii iweze kusimama na vijana na vijana hawa na kuwapa nguvu katika huu mchakato mzima wa kutafuta fedha za kukimu maisha yao. Ahsante Mheshimiwa Spika?

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani)**:** Thank you Honourable Katana. Yes Honourable Mariam Baimu?

Hon. Baimu: Mwanzo ningependa kushukuru Mheshimiwa Spika kwa kunipa fursa hii, pili ningeweza pia kumshukuru Mheshimiwa Amriya kwa kuleta hoja hii. Nafikiri sote tunafahamu kwamba vijana wetu ndio viongozi wetu wa kesho na hii katika kupeleka mambo kupeleka na bodaboda ama hizi tuktuk ni moja wapo ya kutafuta ajira ili waweze kujikimu kimaisha. Lakini ni jambo la kusikitisha Bwana Spika hawa watoto wengi tunaoona kama vile wenzangu walivyotangulia kusema wao leo wanajifundisha katika vichochoro kupeleka hizi bodaboda, kesho wako kwa barabara hawana vibali vya kuweza kupeleka. Kwa hivyo si uongo hawajui zile *traffic rules* ambazo zinatakikana mtu uzielewe unapopeleka vitu hivi hivyo basi kitu ambacho naonelea ni cha sawa ni kwamba kama hawa wafadhili watapatikana hao watoto waweze kukusanywa wale ambao hawajaenda *driving school* wapelekwe ili waweze kujifunza sheria za barabara na waweze kuelewa ni nini wanatakikana wafanye wakati wamebeba abiria manake si uongo tunaona kuna *ward special* pale Coast General ambayo hawa watu wanaovunjika miguu wa bodaboda wanalazwa pahali hapo. Kwa hivyo mimi naona ni Hoja ya sawa na ni vizuri, mimi naiunga mkono kama Mheshimiwa Mama Maryam. Ahsante.

[Applause]

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani)**:** Yes, Honourable Maimuna Salim, she is the senior most Member in this Assembly.

Hon. Maimuna Salim: Mheshimiwa Spika ahsante sana nakushukuru kwa kunipa fursa hii, nimesimama kuchangia Hoja hii ilioletwa na Mheshimiwa Amriya Boy Juma Boy. Mheshimiwa Spika tunajua ya kwamba sote tuwasafiri wa bodaboda kwa sababu katika njia hii ama nyengine uwe na gari lakini saa zengine umefika na gari kuchelewa na bodaboda wanaweza kupenya. Kwa hiyo ni vizuri waende katika mafundisho, wakishaenda katika mafundisho watakuwa na vibali vyao kama Wakenya wengine.

Hii ni kwa sababu wengi wanapeleka lakini hawana vile vibali kwa hiyo ni vizuri wakienda kwa mafunzo wapate vibali kama Wakenya wengine, pili ni vizuri tuwafikirie katika kila Wodi *at least* wawe na *Sacco* zao itakuwa ni rahisi Mheshimiwa kujua ni wangapi ambao wameenda mafunzo ya udereva na ni wangapi ambao hawajaenda mbali ya ile *umbrella* yao ni kwa sababu najua boda boda wote wako kwa *umbrella* lakini pia tukiwaweka kwa Wodi itakuwa ni vizuri sisi kama Waheshimiwa tunaweza kuwa *monitor*. Jengine ambalo litazungumzia ni kwamba pia tunawaombea Mungu akitujaalia sisi kama Wabunge tulete na tung'ang'ane ili waweze kupata zile *shades* kwa sababu hawana *shades* wanasimama mahali wanapigwa na jua na wale ni binadamu kama sisi na wakati wa siasa sana huwa tunawatumia. Kwa hiyo namshukuru Mheshimiwa Amriya kwa kuleta Hoja hii kwa kuweza kuwafikiria wale vijana ni vijana muhimu sana Mheshimiwa Spika na tukumbuke ya kwamba hawa ni vijana ambao wanapeleka meseji mashinani tutakapoweka *shade*, uwapeleke *driving* wawe na vibali kamili kusema la ukweli basi wewe umejitengenezea siasa yako ya 2027. Kwa hiyo mimi naunga mkono na naomba tushirikiane ili tusaidiane vijana wetu. Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipa fursa hii.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani)**:** Thank you. Yes, Honourable Fatuma Swaleh Mote?

Hon. Fatuma Swaleh: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kuweza kunipa fursa hii. Kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu muumba Mbingu na ardhi pasi na kizuizi; pili wale Waheshimiwa ambao watakuja katika hili Bunge manake mimi ni Mwenyekiti mdogo wa afya wanasema wakizungumza watatoa vitu vyengine na hichi ni chombo ambacho twatumia sote ikiwa wajua utazungumza utatoa vitu kwenye pua yako afadhali uende hospitali ama ukae nyumbani tusiweze kuambukizana. Mheshimiwa Spika nimesimama kidete kuunga mkono mjadala ulioletwa na Mheshimiwa ambaye ni wakili mwenye akili; ukiangalia mimi katika Wodi yangu ya Kadzandani ni Wodi ambayo ina maskini wengi na hizo bajaji ama bodaboda sisi ndio huwa tunatumia na ukiangalia watoto wengi siku hizi wanatumia bodaboda ama bajaji kwenda shuleni na watu wengi pia wanatumia bajaji hata kwenda kazini kama alivyozungumza Mheshimiwa mwenzangu jirani anakwambia ukienda katika *ward* utaona watu wengi sana wamepata majeraha na mengi yanatokana kwa usafiri wa bajaji ama tuktuk.

Mheshimiwa Spika, vile vile ningependa Mheshimiwa pia aweze kuongezea kwamba hapa Kaunti ya Mombasa sisi tuna sehemu kubwa sana ambayo hiyo sehemu yaweza kutoa mafunzo yaani kukawekwa kama wenyewe wazungu wanaita *college* yaani mahali ambapo watoto wanaweza kupata masomo na hiyo sehemu mimi najua *mia fil mia* huijui lakini naweza kukumbusha hiyo sehemu iko kule *fire* Likoni. Ile sehemu Mheshimiwa Spika ni kubwa sana na pale pia sisi twaweza kuchukua vijana tukawafanyia mafunzo na vilevile huku tukiwafanyia mafunzo na sisi kama Kaunti tunapata kipato cha kuongeza ushuru. Mheshimiwa Spika, tukiangalia wapelekaji bajaji ama tuktuk ni watu ambao ni wanyonge na wanajikimu maisha yao ama kipato chao wanapata katika hizo kazi na vile vile ningeomba nafikiri Mombasa tuna matajiri wengi sana wale ambao wanauza bajaji na tuktuk waweze kuwasaidia hawa vijana ili waweze kupata mafunzo ili Mombasa Kaunti tuishi kwa usalama. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani)**:** Thank you. Yes, Honourable Frankline Makanga?

Hon. Makanga: Ahsante Mheshimiwa Spika kwa fursa hii na pia nimpongeze Mheshimiwa wakili Amriya Juma Boya kwa kuleta *Motion* hii katika Bunge letu. Mheshimiwa Spika, niruhusu kwanza nianze na kuwarekebisha Waheshimiwa wenza ili inapoenda katika nakala za Bunge hili ieleweke kwamba si *ward* nambari 7 ila ni *ward* namba 8 ndio *ward* inayoshughulikia masuala ya mifupa na si watu wa bodaboda kama inavyosemekana, japo masuala mengi ya wale ambao wamelazwa katika *ward* hiyo wengi huwa wamepata ajali kutokana na bodaboda. Kwa hivyo wasiite *ward* ya bodaboda hakuna *ward* inayoitwa hivyo katika hospitali yetu na *ward* namba 8 ndio *orthopedic ward* na namba 7 ni *surgical ward* na kwa sababu mara nyingi wanaumia huhitaji upasuaji ndio maana labda tunawapata pale. Waheshimiwa kwa hivyo ili tu kwa sababu ya kesho yake tusije tukatokea katika mkutano wa umma ambapo tuko na wale ambao wako katika ile hospitali wakaona hatufahamu ni vizuri tuwe na huu ufahamu uweze kutusaidia. Mheshimiwa Spika, mimi nasimama kuunga Hoja hii na zaidi mahala ambapo tumesema kuweza kuwawezesha vijana wetu, na mbali na vijana wetu pia tuko na mama zetu ambao kwa sasa wanafanya hii kazi ya bodaboda tuko pia na baba zetu ambao licha kwamba wamepitisha umri wa miaka 35 lakini hii ndio kazi wamesomeshea watoto wao na wengine wao Mheshimiwa Spika wako katika Bunge hili ambao wazazi wao huamka asubuhi wakaenda wakatafuta riziki katika sekta hii na hivi leo wameweza kufikisha watoto wao hapa wanaitwa Waheshimiwa.

Mheshimiwa Spika, mimi naunga mkono Mswada huu kwa kikamilifu. Nafikiri mwenzangu hapa nyuma yangu hua anaunga na asilimia lakini mimi na leo muniruhusu niunge na asilimia, kwamba naunga kwa asilimia mia moja ili kwamba hawa vijana wetu ama hii sekta tuweze kuiangazia kwa mda huu na kipindi hiki yale ambayo yamewekwa katika hii ni sehemu ya zile *function* ambazo ni za serikali ya Gatuzi la Mombasa ambapo sisi tunafaa kuwajibika. Hawa wenye hizi biashara za pikipiki ni jukumu letu sisi sio kwa sababu ya siasa ya kesho lakini ni haki yao Kikatiba kwamba sisi tuhakikishe wamewekewa vile vibanda vya kuwastiri wakati wa jua na mvua. Mara nyingi Mheshimiwa Spika tunaona vijana wetu wengi wakihangaika wakati jua ni kali na wakati kunanyesha hawana mahali pa kujistiri wakati hii ni kati ya kazi ambazo kulingana na Katiba ya Kenya ya 2010 *schedule 4, part b* Mheshimiwa Spika imesema kwamba wajengewe mahali ambapo zinaitwa *shades.*

Kwa hivyo sisi kama Waheshimiwa tunaposukuma yale mengine ambayo labda tumeyaona mbele yetu na katika macho yetu kwamba yanayostahili tujue kwamba hili ni jukumu letu kama serikali kuhakikisha kwamba wana bodaboda wamelindwa, wamewezeshwa na wamesaidika kuinua maisha yao kwa sababu pia kwa kiwango kikubwa wanachangia pakubwa sana katika uchumi wa nchi hii, katika uchumi wa Gatuzi la Mombasa na pia katika usalama tumewaona wakitusaidia sana kuweza kupambana na uhalifu katika jamii. Kwa hayo mengi nasimama kuunga mkono. Ahsante.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani)**:** Honourable Members. Yes, Honourable Mbelle.

Hon. Mbelle: Shukran Bwana Spika. Kwanza nipongeze alieleta Mswada huu na nafikiri umekuja katika wakati sawa kulinganisha kwamba katika Kaunti yetu ya Mombasa, sehemu zile ambazo zimekuwa za kuandika watu kazi zimekuwa chache na wengi vijana wetu wameiweka katika *sector* hizi za bodaboda na tuktuk. Sasa Mheshimiwa Spika kwanza ningependa kuambia Jumba hili kwamba jana nilikua katika hospitali ya *Coast general* nilienda pale kuangalia mmoja wa watu wanaishi katika wadi yangu na bahati mbaya ikawa ni mtu mlemavu jana aligongwa na bodaboda na akavunjwa miguu yote miwili.

Na mtu yule pamoja na dereva wote wako hospitali pale wamelazwa lakini cha kutamausha ni kwamba katika wote wale wawili hakuna ambae alikuwa na bima ya kuweza kumsaidia mwenzake katika maswala ya kutibiwa ama ya kujisaidia mwenyewe. Kwa hivyo langu ni kuomba ya kwamba tunapoazimia kutekeleza yale ambayo tumeleta katika hoja hii na hasa katika serikali ya Kaunti, moja wapo ya vitu ambavyo tunafaa tuweke ni kuhakikisha kwamba kila mwana boda boda ama kila mwenye tuktuk, aidha tutamuwezesha kupata ile NHIF ama tuweke sheria ya kwamba mtu yoyote ambae anafanya kazi ya bodaboda ama tuktuk lazima awe na bima ya NHIF iwapo bahati mbaya na hatuombi bahati mbaya imepatikana ajali amegongwa mtu awe na uwezo angalau wa kujikimu, wengi wa Waheshimiwa katika Bunge hili najua hakuna ambae chini ya mwezi mmoja hakosi mtu wa boda boda, hakosi mtu wa boda atamwambia nisaidie na pesa niende hospitali lakini ingekuwa wote wako na zile NHIF wanaweza kujipeleka hospitali na kuweza kujitibu na kubakia salama. Patakuwa na sheria, patakuwa na mengi ambayo tutaweka lakini tunavyoambiwa ajali saa zengine haina kinga kwa bahati mbaya ikapatikana atakua anaweza kujisaidia. Kwa hivyo naunga mkono mia *fil* mia na ahsante wakili Amriya. Shukran.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani)**:** Honourable Mwaka.

Hon. Mwaka Bakari: Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti. Yale ambayo nilikuwa nataka kusema pia yamesemwa na Mbelle lakini bado na mimi nitaweka sauti yangu na kuweza kuunga mkono hoja hii ambayo imeletwa na Mheshimiwa Amriya Juma Boy. Kwa kusema kweli vijana hapo ndio ajira, ajira hakuna na pindi watakapokuwa wanafanya ile mambo na bodaboda sio eti ni kukosa kazi, ile ni kazi kwa sababu wengi wao wanapata kuweza kujisaidia na kujikimu kimaisha kwa sababu ya kazi hii. Lakini pia vilevile tunataka kweli tuweze kuwapatia mafundisho ya *driving license* wengi wao hawana *driving license*, wao wanajifundisha mtaani siku moja tu ama dakika tu masaa mawili tayari amekuwa yeye ni dereva, hajui zile sheria za barabara na wala hajui kwamba hii nikifanya itakuwa ni shida hapo pia wanapatia fursa *traffic police* wa kuweza kuwadondoa kwa sababu yeye mwenyewe hajui vile ambavyo anaendesha ile pikipiki. Kwa hivyo mimi naunga mkono hoja hii ili iweze kutiliwa maanani na kuwekwa nguvu ii waweza kupata mafundisho hayo ya *driving school* na pia vilevile sio *driving* pekee hata pia tunataka tuwapatie darasa tuwafundishe mafundisho dereva anatakikana vile yuko. Kwa sababu mara nyengine unapanda boda boda unamsimamisha lakini ukipanda hicho kikoti chanuka kabisa hajaoga karibu siku tatu. Kwa hivyo pia vilevile ni mafundisho ya usafi akijua kwamba yeye anabeba abiria pia anatakikana kubeba abiria vilevile pia wataka wapewe *counseling* ya kwamba vile wanabeba watoto wengi wao wa boda boda hua wanabaka watoto, wengineo pia wanatumika vibaya kwa mambo ya uwizi. Hivyo basi, hizi boda boda zimeletwa lakini zina sifa tofauti tofauti, lakini pindi tutakapo wapata na kuweza kuelimisha wengi wao watajua hii ni kazi na akipenda kazi ile ataweza kuwajibika na yale masharti ambayo yanatakikana ili iweze kumjenga kimaisha kazi hii. Ahsante sana Bwana Mwenyekiti mimi nasimama kuunga mkono hoja hii ilioletwa na Mheshimiwa Boy.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani)**:** Thank you Honourable Mwaka. Yes, Honourable Hassan.

Hon. Hassan Mohammed: Ahsante sana Bwana Spika kwa kuweza kunipatia fursa adhimu fursa muhimu ya kuweza kuchangia hoja ambayo imeweza kuletwa na jirani yangu Amriya Boy Juma.

Kuhusiana na Mswada ambao uko hapa ndani ya Jumba hili; nikizungumza kama Mwenyekiti katika Kamati ya uchukuzi na miundo msingi napenda kupendekea mambo muhimu ambayo lazima yazingatiwe kwa sababu ni mastaajabu yangu ya kwamba kila kinacholetwa katika Bunge hili kinapita bila kupingwa. Sasa sijui ni mapenzi ama tunataka maendeleo, ni mengi tu ambayo yameweza kuletwa na yote yamepita lakini katika utenda kazi bado tunaomba Mungu atupatie nguvu kuweza kuimarisha haya yote. Hili jambo la boda boda, tuktuk na vitu vingine kwa idadi naona kwamba ndani ya Mombasa sisi abiria ndio hatupo lakini hivi vyote vipo, ndio unaona kwamba unapofika katika steji boda boda tano zinaweza kukuvamia wewe abiria mmoja. Kama tukiwa waangalifu zaidi naweza sema kuthibiti hawa walioko ni kitu muhimu zaidi kuliko kuongeza mengine, kwa sababu ikiwa tutaongeza tutakuwa tunaongeza madhara. Juzi katika kata yangu ndogo ya Magogoni, nasikitika kwamba hizi boda boda ziliweza kutumika mpaka tukaweza kupoteza uhai wa mtu mmoja na karibu takriban wanane wapo katika hospitali ya Makadara ambapo ndugu yangu Mheshimiwa Ogutu, kama Mwenyekiti wa Kamati ya Afya anazidi kunisaidia kuwatoa maana yake mpaka sasa wametolewa nje. Boda boda hizi zinatumika katika njia tofauti ni lazima tuwe waangalifu na tuwe makini sana, ikiwa boda boda tutazidi kuwapatia nguvu basi tuangalieni ni jinsi gani nguvu tunawapatia. Je tunawapatia stendi? Tunawapatia leseni? Tunawaangalia ni jinsi gani kuimarisha kuwatoa katika njia ya boda boda kuwapeleka katika njia nyengine. Ikiwa ana boda boda moja ama mbili, ni jinsi gani tunaweza mpatia nguvu akawa na tuktuk na huyu mwenye tuktuk tumtoe hapa tumpeleke kwengine lakini tukizidi kuwaingiza katika sekta hii Mheshimiwa kulingana na steji zetu, kulingana na barabara ambazo mpaka sasa tumeahidiwa na bado hatujajua mwelekeo tunaomba Mungu zianze kufanyiwa kazi, jamaa tuwe waangalifu sana upande huu. Kule kwetu sijui huku mjini boda boda ni kidogo sana hata katika kata hii nafikiri sidhani kama zipo zinafanya kazi lakini kule kwetu mimi binafsi, hawa watoto ni lazima tuwe waangalifu Bwana Spika ikiwa tunapitisha mambo fulani katika Bunge hili kwa sababu mimi sijui niuunge ama nipinge lakini mimi kama Mwenyekiti wa Kamati ya Uchukuzi na Miundo Msingi nitakaa na Kamati yangu tulijadili hili kisha, hao wengine kama wataunga wacha waunge Bwana Spika lakini mimi ilikuwa ni maoni tu ndugu yangu hizi boda boda hazitumiwi kwa uzuri boda boda hizi. Ahsante sana.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani)**:** Thank you. Yes, Honourable Mbaya?

Hon. Khamis Salim Mbaya: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipatia fursa hii, na kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia sisi kuwa ndani ya Jumba hili tukiwa na afya tele tele. Mimi nataka niwe mfupi wa maneno nikisema shuka haiwi kaniki na kaniki haiwi shuka. Naliunga mkono swala hili asilimia 90 kwa sababu halina mjadala wa zaidi. Ahsanteni. Shuka haiwi kaniki na kaniki haiwi shuka.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani)**:** Thank you Honourable Mbaya. Honourable Members I can see you have exhausted this Motion; I now call upon the mover of the Motion to respond yes Honourable Amriya?

Hon. Amriya Juma: Thank you Honourable Speaker for allowing me to respond. I wish at this point to thank the Honourable Members for their contribution towards the Motion, it is clear that this matter of boda bodas and tuk tuks are closer to most of the Members heart and at this point I think it is only necessary for us to move very quickly and going to policy making because the statistics say that Mombasa has over 7,000 registered tuk tuks and over 10,000 of boda bodas.

But the statistics on boda bodas is unknown because there is no proper policy on the same. So maybe the House should not stop at the Motion but we can go ahead and do the different laws and I think the issue of NHIF is very important for this sector. If maybe they could be given priority basis it is going to really impact on our society at large just the way the motor vehicles are done insurance and all that. So, a lot is yet to be done and we have so much on our table, so I urge this Honourable House to support the Motion and I also urge the Chair of Implementation to see to it that there is stakeholder engagement and see to it that this Motion and further policies or further Motions to see the light of the day and for the benefit of this good society of ours. Thank you, Mr. Speaker.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani)**:** Thank you Honourable Members. Honourable Members, before I put a question, I would just like to wish you happy Valentine's Day! Having said that Honourable Members, I now put a question that the Motion by Honourable Amriya Juma Boy on *Partnership between County Government to Build the Capacity of Youth, Tuktuk and Boda boda Drivers* be approved in this House.

[Question put and agreed to]

ADJOURNMENT

Honourable Members, the House stands adjourned until Wednesday, 15th February, 2023 at 10:00a.m.

The House rose at 3:24a.m